



# LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Block 44, Plot 508 & 509, Kijitonyama,  
P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA • Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037,  
E-mail: [lhrc@humanrights.or.tz](mailto:lhrc@humanrights.or.tz) Website: [www.humanrights.or.tz](http://www.humanrights.or.tz)

*for a Just and Equitable Society*

**Kumb. Na.:** LHRC/PRESS/VOL.II/95

**Tarehe:** 15 Aprili 2015

## **TAMKO KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU KAULI YA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI MH. MATHIAS CHIKAWA KUTISHIA KUZIFUTA TAASISI ZA KIDINI ZITOAZO MATAMKO KUPINGA KATIBA INAYOPENDEKEZWA**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimepokea kwa masikitiko makubwa tamko lililotolewa na Waziri wa Mambo ya Ndani Mh. Mathias Chikawe ambalo linalenga kuzuia na kufuta taasisi za kijamii na kidini kutokana na kutoa matamko ya kuikataa Katiba Inayopendekezwa. Kauli hiyo ilitolewa tarehe 14/4/2015 na kuelezea dhamira ya Serikali kufungia taasisi hizo kuanzia tarehe 20/4/2015.

Kimsingi kauli ya Mh. Mathias Chikawe ina dhamira ya dharti kabisa ya kupokonya uhuru wa kutoa maoni kwa makundi mbalimbali juu ya Katiba Inayopendekezwa, kinyume kabisa na misingi ya utengenezaji wa Katiba ambao unahitaji mchango wa watu wengi zaidi ili kufikia Katiba iliyo bora na yenye ushiriki wa makundi mbalimbali hapa nchini.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu pia kinashangazwa na kauli ya Mh. Waziri kwa kuwa inaonyesha lengo la kuondoa makundi ya kijamii na kidini kutoa mitazamo yao kuhusu Katiba Inayopendekezwa. Katika hatua za utengenezwaji wa Katiba hii Inayopendekezwa, kuliundwa Bunge la Katiba ambalo ndani yake kulikuwa na kundi la 201 ambalo lilihusisha Taasisi za Kijamii sambamba na zile za kidini. Kwa msingi huo Serikali iliona umuhimu na mchango wa taasisi hizi katika mchakato wa uundwaji wa Katiba mpya, iweje sasa Waziri wa Mambo ya Ndani anaibuka na kutoa onyo kwa makundi haya kutotoa matamko kuhusu Katiba wakati kimsingi nayo ni sehemu ya utengenezwaji wa Katiba ya nchi.

Taasisi za dini ni vyombo ambavyo ndani yake kuna wananchi wengi ambao ni wapiga kura watarajiwa wa kura ya maoni, vile vile ifahamike kuwa viongozi wa taasisi hizi za dini hawapotezi haki yao ya kuzungumzia masuala ya Katiba kwa sababu tu wao ni viongozi wa taasisi hizi.

Ikumbukwe pia kuelekea kura ya Maoni kutakuwa na pande mbili nazo ni wale wanaopiga kura ya NDIO na HAPANA, hivyo basi si vyema kumnyima uhuru mtu anayeona kuwa ana haki ya kupiga kura ya HAPANA kwa Katiba Inayopendekezwa, kwa kuwa huo ndio msimamo wake na ni msingi wa demokrasia. Hivyo basi si vema kwa mtu au kundi lolote kutoa vitisho vya aina yoyote ile hatimaye kudhulumu haki hiyo ya msingi ya Binadamu kupiga kura na kuchagua kile anachokitaka.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapinga kauli hiyo ya vitisho iliyotolewa na

### **Board of Directors:**

Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Athanasia Soka (Adv) - Vice Chairperson, Dr. Helen Kijo-Bisimba - Secretary, Mr. Francis Stolla (Adv),  
Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.